

# **OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

**(OR-TAMISEMI)**

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA.**

SHULE YA SEKONDARI HANIHANI,

S.L.P 61

**IGUNGA**

**Simu Na. 0621-176785**

03/12/2020

**Kumb. Na. HNS.S/KDT.1/2021/01**

**Mzazi/Mlezi wa.....**

**Shule ya Msingi.....**

**Yah: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI HANIHANI WILAYA YA IGUNGA MKOA WA TABORA MWAKA 2021.**

### **1. Utangulizi.**

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021**. Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Mwanao anatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25/01/2021** ndani ya siku **14**.

### **2. Mambo muhimu ya kuzingatia**

#### **2.1 Sare za Shule**

##### **(a) WASICHANA**

- (i) Sketi mbili **(2)** za rangi ya Udongo zenyé marinda yasiyopungua nane inchi **1 $\frac{1}{2}$**  ya kuelekea upande mmoja na urefu uzidi magoti kwenda chini.
- (ii) Shati mbili nyeupe **(Tetroni)** mikono mifupi.
- (iii) Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu wala urembo(Jozi mbili).
- (iv) Soksi ndefu nyeupe
- (v) Viatu vya michezo (raba nyeusi) Jozi moja.
- (vi) Hijab inaruhusiwa iwe ya heshima na ifanane na sare za shule.
- (vii) Sweta rangi ya kijivu.
- (viii) T-Shirt ya kijivu yenye kola **(yenye nembo ya shule ya sekondari Hanihani)**

(b) **WAVULANA**

- (i) Suruali mbili za rangi ya Udongo zenyne mifuko miwili pembedi na mmoja nyuma na ziwe na marinda mawili tu, pia zisiwe za mtepesho na zisiwe za kubana (**Modo**).
- (ii) Shati mbili nyeupe Teton mikono mifupi.
- (iii) Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino wala urembo (**Jozi mbili**).
- (iv) Soksi nyeupe.
- (v) Viatu vya michezo (**raba nyeupe**) Jozi moja.
- (vi) Sweta rangi ya kijivu.
- (vii) T-Shirt ya kijivu yenyne kola (**yenye nembo ya shule ya sekondari Hanihani**)

**2.2. Mahitaji muhimu kwa mwanafunzi.**

- (i). Daftari kubwa (**Counter Book 2Q**) kumi na mbili (**12**)
- (ii) Daftari ndogo **12** kwa ajili majaribio ya kila wiki
- (iii) Kalamu
- (iv) Penseli
- (v) Rula
- (vi) File moja (**Spring File**)

**3. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria **Na. 10** ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundu yenyne dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya **Rais-TAMISEMI** yenyne jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo pamoja na kanuni na taratibu za shule zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria.

**3.1 ZINGATIA YAFUATAYO**

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- (g) Kuuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;
- (i) Kutunza mali za umma.

**3.2 makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa masomo.**

- (a) Wizi.
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- (h) Kuoa au kuolewa
- (i) Kutoa mimba.
- (j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (k) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (l) Kuwa na simu ya mkononi
- (m) Kuwa mtoro

**3.3 SEHEMU ZILIZOKATAZWA**

- (a) Kuingia nyumba za kulala wageni(Guest House)
- (b) Kumbi za starehe
- (c) Sehemu za kuuzia pombe
- (d) Nyumba za walimu
- (e) Maabara isipokuwa kwa kibali maalum

**4. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

1. Medical examinational form amabayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara atakaporipoti shuleni.
2. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
3. Fomu ya mzazi ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule
4. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI HANIHANI.**

.....  
**MWL. CHRISTOPHER SHIRIMA  
MKUU WA SHULE**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**HANIHANI SECONDARY SCHOOL**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by medical officer in respect of all FORM-1 entrants.

Please examine the under mentioned student as to his/her physical and mental fitness for his/her full time student of the school.

Student's name.....

Age.....Sex.....

Blood found(red and white).....

Stool examination .....

Urinalysis.....

Venereal diseases test.....

T.B test.....

Eye test.....

Spleen.....

Abdomen .....

Urine for pregnancy.....

**ADDITIONAL INFORMATION(in any) e.g physical defects, impairment(s) e.g Arm, Leg e.t.c**

Infection chronic or family diseased etc.....

I certify that the above is fit to peruse her/his education as stated above

Signature .....Designation.....

Station..... Date.....

## **SHULE YA SEKONDARI HANIHANI**

Fomu hii iiazwe na mzazi/ mlezi wa mwanafunzi ili kukiri kukubaliana na sheria za shule, kanuni, kulipa michango na maelekezo mengine yatolewayo na shule kwa mwanafunzi na iletwe siku ya kuripoti shuleni.

### **AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi .....ninaahidi kuwa nitafanya bidii katika masomo yangu muda wote niwapo shuleni na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Naahidi pia sitashiriki kwa aina yoyote ya mgomo, fujo, uchochezi au makosa ya jinai.

Saini ya mwanafunzi.....Tarehe.....

### **AHADI YA MZAZI**

Mimi .....ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi .....wa kidato cha .....

Naahidi kuwa nimeelewa maelekezo yote ya shule na ninaahidi kuwa nitatoa ushirikiano wakati wote kwa uongozi wa shule katika kumpatia kijana wangu

.....  
Malezi bora. Aidha nakiri kukubaliana na sheria za shule, kanuni na kukubaliana kulipa michango yote na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule muda wote wa uanafunzi wa kijana wangu. Aidha sintasita kutoa taarifa kwa uongozi wa shule juu ya mwenendo mbovu wa kijana wangu kwa lengo la kumrudi.

Saini ya Mzazi/Mlezi.....

Tarehe.....